

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## OFISI YA RAIS

### SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Kumb. Na. JA.9/18/01"C"/18

23/01/2025

### TANGAZO LA KUITWA KAZINI

Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma anapenda kuwataarifu waombaji kazi wa nafasi mbalimbali waliofanya usaili kati ya tarehe **02-10-2024** na tarehe **17-12-2024** kuwa matokeo ya waombaji kazi waliofaulu usaili huo ni kama yalivyoorodheshwa katika tangazo hili. Orodha ya majina haya pia inajumuisha baadhi ya wasailiwa waliokuwa kwenye kanzidata (**Database**) kwa kada mbalimbali ambao wamepangiwa vituo vya kazi baada ya nafasi kupatikana.

Waombaji waliofaulu usaili wanatakiwa kuchukua barua za kupangiwa kituo cha kazi katika **Ofisi za Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma zilizopo katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kwenye Majengo ya Dkt. Asha Rose Migiro, Masjala ya wazi ndani ya siku saba kutoka tarehe ya tangazo hili na baada ya hapo barua ambazo hazitachukuliwa na wahusika zitatumwa kupitia anuani zao za Posta.**

Aidha, waombaji kazi waliofaulu usaili na kupangiwa kituo cha kazi wanatakiwa kuripoti kwa Mwajiri katika muda ambao umeainishwa kwenye barua za kupangiwa kituo cha kazi wakiwa na vyeti halisi (**Originals Certificates**) za masomo kuanzia kidato cha nne na kuendelea ili vihakikiwe na mwajiri kabla ya kupewa barua ya Ajira. Kwa wale ambao majina yao hayapo katika tangazo hili watambue kuwa hawakupata nafasi/hawakufaulu usaili, hivyo wasisite kuomba kwa mara nyingine nafasi za kazi zitakapotangazwa.

## **MUHIMU:**

Wanaokuja kuchukua barua za kupangiwa kituo cha kazi wanapaswa kuwa na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi; Vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na:- **Kitambulisho cha Uraia, Hati ya kusafiria, Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, Kitambulisho cha Mpiga kura au Leseni ya Udereva.**

NA	MAMLAKA YA AJIRA	KADA	MAJINA YA WALIOITWA KAZINI
1	Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)	DEREVA DARAJA II	1. VICENT MGAA TINDIKALI 2. EDWARD ANTHONY EDWARD 3. HUSSEIN SULEIMAN HUSSEIN 4. THOMAS DAUDI SANGA
2	Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)	RECEPTIONIST II	1. SHAFII ABDULBASHAR KASHAIJA
3	Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)	ICT OFFICER II (NETWORKING)	1. ELIAS JOSEPH MSUYA
4	Wizara ya Maji	MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA II	1. NELSON NWAKA MWAIPOSYA 2. JAQULINE JOSEPH MVUNGI 3. CRESENSIA BELTOD NYAULINGO 4. MOSES JOFREY JACOB

LIMETOLEWA NA;

KATIBU

SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA